### Kuzuia

- Unashauriwa kupanda mbegu zinazostahimili ugonjwa huu.
- Usafi wa shamba na kilimo mzunguko wa mazao panda mazao ambayohayaathiriwi na ugonjwa huu.

### Wadudu

- Adui mkubwa wa dengu kwa upande wa wadudu ni funza wa vitumba, huyu hushambulia vitumba na mbegu changa za dengu.
- Huweza kupunguza mazao kwa kiwango kikubwa.

### Kuzuia

Tumia viuatilifu kumuangamiza funza wa vitumba kulingana na ushauri wa Afisa Ugani-kilimo uliye karibu naye.

### Panya


Panya pia hushambulia sana dengu kwa kula mbegu.

### Uthibiti

Weka mazingira ya shamba katika hali ya usafi, haribu vyanzo vyote vitakavyokuwa makazi ya panya, vichaka, mashimo n.k.

### Uvunaji:

- Mimea inapofikia kuvuna inatakiwa kuvunwa mapema, kuwahi sana au kuchelewa kuvuna kunapunguza ubora na kiwango cha mbegu, ukiwahi mbegu hazitakuwa bora kwani zitakapokauka baadaye husinyaa hivyo kupunguza uwezo wa kuota na kuhifadhika.
- Ukichelewa zinaweza kushambuliwa na panya na ndege. Pia zinaweza kupasuka na kutawanyika shambani.
- Ni vizuri kuvuna asubuhi kabla jua halijawa kali kuepuka kupasuka na mbegu kutawanyika kutokana na kupigwa jua kali.
- Vuna tumba mojamoja au ng'oa shina nzima kusanya pamoja na sambaza kuweka katika eneo lililotayarishwa.
- Turubai, jamvi au uwanja maalum kwa kupigia. Ziache mbegu zipigwe jua siku mbili kabla ya kupiga usitumie vitu vizito wala nguvu ya ziada unapopiga ili kuepuka kupasua mbegu.



**Picha:** Zao la dengu shambani

### KUPETA NA KUCHAMBUA

Peta na chagua mbegu toa takataka zote, mbegu zilizopasuka na mbovu, mabaki ya majani mimea na udongo. Unaweza kutumia chekecheo ili kuondoa mbegu ndogo ndogo

### KUHIFADHI

- Tunza katika eneo lenye hewa ya kutosha na kavu, unaweza kuweka kwenye magunia au mifuko ya ujazo mbalimbali kutegemea na uwezo wako, kumbuka kuhifadhi vizuri huzuia wadudu waharibifu ghalani.
- Pia inulia chanja yako mifuko yako isikae sakafuni, tumia mbao, miti au vifaa vyovyote vitakavyosaidia.
- Unashauriwa kuchanganya dawa kwa mbegu ambayo imepata soko, ushauri wa uchanganayaji dawa unaweza kuupata kwa mtaalam husika aliyekaribu.

**TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA**

TARI
Transforming Agriculture

# KILIMO BORA CHA DENGU








KWA MAWASILIANO;
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)
Kituo cha Ilonga
S.L.P 33, Kilosa Morogoro - TANZANIA
Simu: +255736623283
Barua pepe; cdilonga@tari.go.tz
Tovuti; www.tari.go.tz



TARI Transforming Agriculture
BILL & MELINDA GATES foundation
USAID
CIMMYT
AVISA Healthier and Prosperous Africa


CamScanner

## UTANGULIZI

Dengu ni zao la jamii ya mikunde ambalo umuhimu wake katika jamii unafanana na mazao mengine katika kundi hili, kama Maharange, Kunde, Mbaazi, Soya n.k.

Dengu kutumika kama mboga , unga wake hutumika kutengeneza vitafunwa kama bajia n.k.

Pia dengu ni zao la biashara huuzwa kwa wanunuzi ambao husafirisha nchi za ng'ambo.

Zao hili lina sifa za ziada za kukua kwa unyevunyevu ulioko shambani, haihitaji mvua nyingi.

Hupandwa mwishoni mwa mvua za masika mara baada ya kavuna mahindi, mpunga n.k.

### HALI YA HEWA

Dengu haihitaji mvua nyingi inakuwa kwa unyevunyevu wa shambani na hustawi vizuri katika udongo wa mbuga sehemu ambazo hazituanishi maji iwapo mvua itanyesha.

Udongo wa mbuga unauwezo wa kuhifadhi unyevunyevu/maji kwa muda mrefu hivyo kuwezesha dengu kustawi.

### MWINUKO

Maeneo yenye mwinuko kati ya mita 1500 hadi 2,700 kutoka usawa wa bahari hufaa kwa kilimo cha dengu

### UDONGO

Dengu hustawi vizuri kwenye udongo wenye kiwango cha uchachu (pH) kati ya 6 hadi 7.5 ambao hautuamishi maji

### SIFA ZA SHAMBA LA KUZALISHA DENGU

Kama tulivyokwishaona dengu haihitaji maji mengi hasa wakati wa upandaji. Hivyo inashauriwa kuchagua sehemu ambazo haziruhusu maji kukaa kwa muda pia udongo uwe wa mbuga.

Inashauriwa kutozalisha mbegu katika shamba ambalo msimu uliopita lilllimwa dengu, hii inasaidia kuzuia magonjwa kama mnyauko fuzari na pia kuchanganyikana kwa mbegu za maotea ya mbegu za msimu uliopita.

### UTAYARISHAJI WA SHAMBA

Lima shamba lako katika kina cha sm 15 (inchi 6) na lainisha udongo vizuri.

Hii itasaidia kuweka mazingira mazuri ya uotaji wa mbegu zilizopandwa na pia kusaidia kuchelewesha uotaji wa magugu shambani.

Kazi hii inaweza kufanywa kwa jembe la ng'ombe, jembe la mkono au trekta.

### UCHAGUZI WA MBEGU

Hakikisha unapata mbegu bora ya aina unayotaka kuzalisha kutoka katika vyanzo vinavyofahamika na hakikisha ipo katika ubora unaotakiwa.

Unaweza kupata ushauri kwa mtaalaam wa kilimo aliyekaribu yako iwapo utakuwa na mashaka. Ni vizuri mbegu ikafanyiwa majaribio ya kiwango cha uotaji kabla haijapandwa shambani.

### AINA ZA MBEGU ZA DENGU

Kituo cha Utafiti wa kilimo TARI Ilonga kwa kushirikiana na kituo cha TARI Ukiruguru zinapatikana mbegu bora za dengu zenye sifa mbalimbali; kama ifuatavyo;

"*" Mbegu zenye alama ya nyota hustahimili ugonjwa wa mnyauko fusari

| Aina ya mbegu | Kukomaa (siku) | Mavuno (t/ha) | Rangi ya mbegu | Rangi ya maua |
|---|---|---|---|---|
| Mwanza 1* | 90-100 | 2.4 | Kahawia | Zambarau |
| Ukiriguru 1 | 95-100 | 1.8 | Kahawia | Zambarau |
| Mwanza 2* | 100-110 | 1.5 | Nyeupe/ maziwa | Nyeupe |
| Mwangaza | 100-115 | 1.2 | Nyeupe/ maziwa | Nyeupe |

NB: *Kabuli - Dengu nyeupe huwa ni kubwa na nzito (25 – 40 gm/100 seeds)*

*Deci - Dengu nyeusi/ kahawia – Huwa ni ndogo ndogo siyo nzito sana mfano wake ni dengu za kienyeji sambe sokoni na dengu mawe (20 – 30 kg/100 seeds)*

### UPANDAJI

- Panda katika mistari ili kuweza kupata mimea mingi katika eneo na pia kurahisisha kazi nyingine za shambani kama palizi, unyunyiziaji dawa inapobidi na kuvuna.
- Nafasi kutofautiana kutokana na aina ya mbegu na asili ya makuzi ya mbegu husika.
- Kwa mbegu ambazo hunyooka, ambazo hazitoi matawi mengi panda katika nafasi ya sentimita 30 x 10 panda mbegu mbili. Kwa mbegu ambazo hutambaa/kutoka matawi yanayosambaa pembeni unashauriwa kupanda katika nafasi ya sentimita 40 x 20 panda mbegu mbili.



Picha: Upandaji wa dengu kwa mstari

### MATUMIZI YA MBOLEA

Ni vizuri kurutubisha shamba kwa mbolea za samadi au za viwandani, ushauri wa aina ya mbolea na kiwango chake utaweza kuupata kwa afisa ugani aliyekaribu yako ingawa hiyo itategemea historia na sifa za udongo katika shamba lako.

### PALIZI

- Dengu hukua taratibu siku za mwanzo za ukuaji hivyo uwezo wake wa ushindani na aina yoyote ya magugu katika kipindi cha wiki 6 za mwanzo ni mdogo sana.
- Hivyo unashauriwa kuweka shamba lako katika hali ya usafi katika kipindi hiki, palizi inaweza kufanywa kwa jembe la mkono. Iwapo shamba limeandaliwa vizuri palizi moja inatosha, palizi nyingine zitategemea hali ya magugu shambani.

### MAGONJWA NA WADUDU

- Ugonjwa ambao unasumbua sana zao la dengu ni ugonjwa wa mnyauko fusari, ugonjwa huu husababishwa na fangasi
- Dalili kuu ni kulegea kwa majani na kuelekea chini
- Mmea kunyauka na kufa kabisa
- Weusi katikati ya shina kwa ndani likipasuliwa